# Je umesikia...?

KUWA mjini Bukavu wakaaji na wapitanjia hasa wadereva watishwa bado na hali ya mabarabara ?

Je ? Kwa kuwa tu mashimo yaendelea kuongeza siku kwa siku isiwe tu na maji ya mvua bali pia na hilo shirika la SOZAGEC lenyi kuhusika na kutawanya mirija kwa maji safi ya kunywa baada ya kuchimba mashimo hayo haliyazibi kama inavyohitajika. Mshangao mkubwa ni kuona kama viongozi na wakuu jimboni ambao walihaidia kutengeneza kilometri 20 ya mabarabara mjini wakikabiza kiasi fulani cha feza kwa shirika lenyi ujuzi wa kazi hawajakohoa hata ili raia wangojee matunda mazuri ya feza zilizotolewa na serkali kuu. Na baada ya kupiga kelele na kuziba masikio ya wanachama na wengineo wageni eti kilometri 6 zitatengenezwa upya mjini, leo hii nenda, kuja na kajionee yaliyoko. Popote ni potopoto kweli inayoonyesha kama kazi hiyo yatumikwa kweli ! Sivyo ?

KWAMBA feza zilizotolewa na serkali kuu kwa kutengeneza upya mabarabara na vilalo vijijini zilinyongwa na wananchi wasio na zamiri njema ya kimapinduzi ?

Yasemekana kuwa wengi waliotezamiwa kupewa feza hizo jimboni mwa Kivu ya Kusini walilazimishwa kurudisha kiasi kilichoombwa na "wabwana kuu" kwa manufaa yao wenyewe. Kiasi kingine, wanena wamoja wamoja kati ya watumishi serkalini, chatumiwa kwa nusu ya kazi hizo za mabarabara na kingine chatiwa mfukoni mwa waliokabizwa. Na hiyo baada ya kuitika kweli wakitia sahihi na mhuri wao kwenyi vikartasi vya serkali eti walipata feza zote zilizotolewa.

Na ni hivi imesikika kwenyi redio Bukavu na Kinshasa kama milioni yapata ishirini zimenyongwa na watu wanaojionya kuwa sasa mizimu !

KAMA wakaaji wa Uvira wanungunika kubadilishwa kwa mwenyekiti wa zamani wa mtaa huo ? Labda. Lakini yaliyo kweli ni kusikia kama kiongozi huyo alipendelea sana kusali na kutawanya neno la Mungu nyumbani mwa wakaaji ingawa, mabati (majanja) na paa za wengi kati yao zilirushwa mara na mara na upepo pia na mvua kali. Na toka hapo hakuna hata msaada mmoja uliweza kuwatolea na wanaohusika. Nenda kajionee soko kuu na shule la maelimisho ya ufundi huko. Ambaye atakayeyaokowa si mwengine bali kiongozi wa sasa. Kumbe huko si kiogozi serkalini kaenda bali ni pastori. Aah ?

Tuzungumze

## Adabu kwa wazee

Katika nchi za Ulaya na za Amerika huona watu kuzarau wazee. Kwa siku hizi Wana-Afrika wengi huanza kuiga kigeni. Ndiyo hivo huwasikia mara na mara kuwatusi wazee, kuwazomea na kuwazarau wakiwatendea kwa kanyaro na wakiwajaza aibu.

Hii ni kisasa. Kitendo hiki lakini hakibarikiwe na Mweny'Ezi, nacho moyo wa mababu haukifurahii.

Katika Afrika ya mababu mambo hayakuwa hivi. Mzee, walimpenda na heshima zote walimtolea. Kwani kadiri mtu alikuwa mzee kadiri ile alimiliki busara: hekima, elimu na maarifa ya kila aina vilipatikana kwa mzee ao wazee na yeyote aliyetaka kuongoka maishani alimuendea mzee. Kwetu jina la mzee halina maana mbaya kama vile katika lugha za kigeni. Kule mzee maana yake mtu mwenyi kumalizika, mtu asiye na mafaa tena maishani. Na kwa kusema haki haingekuwa sheria ya kuwakinga wazee wangeuawa katika nchi nyingi ulimwenguni.

Kwetu uzee si kilema na unao maana yake kama elimu na busara. Mara nyingi -hata leo hii- vijana huita mzee mtu ambaye wanaheshimia, yule ambaye awapitae umri na mwenyi maoni kamili ya maisha. Hivi utawasikia mara nyingi kusema:"Naenda kwa mzee Kamulete kumuomba shauri" ingawa yule Kamulete anayo miaka michache tu zaidi yao.

Adabu yetu kwa mzee itaonekana katika maneno tukiepuka kumuambia neno la kumchoma moyo; katika vitendo tukipenda kumsaidia katika shida zake. Tumsaidie hasa kumpenda siku za mwisho wa maisha yake tukijikaza kumsaidia namna zote. Tumkubalishe kama angali mmoja wetu na tumsadikishe kama angali na nafasi yake katika ujamii. Ibada yetu kwa uzee iwe ya kimoyo tukikumbuka kama tutakapokuwa wazee hatutapenda kutendewa kama kafiri ujamii, tukizarauliwa, kutukanwa, kuchekelewa na kutupwa nje!

Kimengele Kimode

KANISA LA ANGLIKANI

## Shemasi Mbusa apewa upadirisho

Mnamo siku ya Mungu, tarehe 10 Desemba 1989, diocezi ya kianglikani ya Bukavu kajipatia padri mpya. Shemasi Mbusa Bangau kapewa sakramenta ya upadrisho kwa mikono ya askofu Dirokpa Balufuga mbele ya umati wa wakristu na wakuu wa serkali kunako Kanisa Mtakatifu Petro mjini Bukavu-Muhungu.

Katika hotuba yake, askofu Dirokpa kamsifu Prezidenti-muundaji wa chama "MPR" na Baba wa taifa, mareshali Mobutu Sese Seko juu ya amani aliyorudisha nchini Zaïre ambamo kuna pia uhuru wa dini. Amani na uhuru zaruhusu serkali na kanisa kujiunga pamoja kwa maendeleo ya jamhuri.

Kwa ngambo yake, liwali Ndala Kasala wa jimbo la Kivu ya Kusini aliyehuzuria binafsi kwa ibada hiyo kanena kama vyeo vyote vyatoka kwa Mweny'Ezi Mungu. Na anatumaini hivi kama padri Mbusa Bangau atajitolea kwa kuadibisha vijana katika mafundisho ya dini na ya chama.

Padri Mbusa Bangau amepata mwaka jana (1988) cheti chake cha ukamilifu wa miaka mitatu ya teolojia kunako ISTEKI (Institut Supérieur de Théologie du Kivu) mjini Bukavu na baadae kahuzuria semina moja ya wataalam wa maendeleo kunako CEFOCAD (Centre de Formation des Cadres pour le Développement).

Mnamo mwezi wa mayi 1989, mwananchi Mbusa Bangau kafanywa shemasi na toka mwezi wa septemba uliopita katajwa katibu wa diocezi ya Bukavu. Wasomaji wetu watakumbuka kama diosezi ya kianglikani ya Bukavu imefungua milango, yake mnamo mwaka wa 1975. Inaundwa leo hii na majimbo manne: Kivu ya Kusini na ya Kaskazini, Kasaï ya Mashariki na ya Magharibi.

Malekera Bahati

# SOMENI DAFTARI

## YA WANAMEMBA

## WA SERKALI WIKI

## IJAYO